Ikiwa utaiamini injili hii ya Yesu Kristo, kwani imani kama ya mtoto mpokee Yesu kwa kuliitia jina lake. Tafadhali fanya hivyo sasa kama kungali na mwaliko wa wokovu. Yohana Mtakatifu 3:36 *"Amwaminiye Mwana yuna uzima wa milele; asiye mwamini Mwana hataona uzima, bali ghadhabu ya Mungu inamkalia."* Ufunuo wa Yohana 20:15 *"Na iwapo mtu yeyote hakuonekana ameandikwa katika kitabu cha uzima, alitupwa katika lile ziwa la moto."*

Kama kijitabu hiki kimekusaidia kumjua Yesu Kristo kama mwokozi wa maisha yako, tafadhali tuandikie, ili tusherekee pamoja nawe.

Hope tract ministry
All tracts are free, as the Lord provides
P.O. BOX 609 ● YORK, SC 29745 ● 803-684-1535
WWW.HOPETRACTS.ORG
Are You 100% Sure? (Swahili) Tract 506



# Una hakika ukifa utaenda mbinguni?

Biblia ni **neneo la Mungu.**

**Mungu asema** sote tuna mwaliko wa kukutana naye tukifa. Waraka kwa Wahebrania 9:27: *"Na kama vile watu wanavyowekewa kufa mara moja, na baada ya kufa hukumu;"* Jambo la muhimu zaidi maishani ambalo waweza kufanya ni kujtayarisha kukutana na Mungu. Je, mtu aweza kuwa na uhakika bila tashwishi yoyote kwamab ataenda mbinguni?

**Mungu asema** unaweza kujua! Waraka wa Yohana wa kwanza 5:13: *"Nimewaandikia ninyi mabo hayo, ili mjue kuwa mna uzima wa milele, ninyi mnaoliamini Jina la Mwana wa Mungu."* Watu wengi hudhani kwamba utu wema utawapeleka mbinguni.

**Mungu asema** hakuna aliye mwema. Warumi 3:10,12b,23 *"Kama ilivyoandikwa, ya kwamba, Hakuna mwenye haki hata mmoja...Hakuna mtenda mema, la! Hata mmoja...Kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu;"*

**Mungu asema** kuna deni la dhambi ambalo lazima lilipwe. Warumi 6:23a *"Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti..."* Yesu alitufia ili tusiende jehanamu. Yohana Mtakatifu 3:16 *"Kwa maana jinsi Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa mwanawe wa pekee, ili kila mti amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele."*

Warumi 5:8 *"Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipoku tungali wenye dhambi."* Yesu alimwaga damu yake ya thamana kusafisha dhambi zetu. Wakolosai 1:14 *"ambaye katika yeye tuna ukombozi, yaani, msamaha wa dhambi."* Siku tatu baada ya kuzikwa Yesu alifufuka kutoka katika wafu.

**Mungu asema** lazima tuliamini jambo hili si kwa akili tu bali kwa moyo wetu wote. Warumi 10:9 *"Kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka."*

**Mungu asema** lazima utubu. Luka Mtakatifu 13:3 *"Nawaambia, Sivyo; lakini msipotubu, ninyi nyote mtaangamia vivyo hivyo."* Hii yamaanisha kukiri dhambi zako, kutoka katika dhambi na kumgeukia Yesu na kumpokea kuwa Bwan na Mwokozi wako. 2 Wakorintho 7:10 *"Maana huzuni iliyo kwa jinsi ya Mungu hufanya toba iletalo wokovu lisilo na majuto..."* Yohana Mtakatifu 1:12 *"Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake."*

**Mungu asema** yeyote aweza kuokoka. Warumi 10:13 *"Kwa kuwa, Kila atakayeliita Jina la Bwana ataokoka."*